**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA MAWASILIANO ARDHI NA NISHATI YA BARAZA LA WAWAKILISHI, KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAAGIZO YA KAMATI YA

MWAKA 2021/2022 - WIZARA YA MAJI NISHATI NA MADINI

**Mheshimiwa Spika,** Kwanza kabisa naomba kuchukuwa fursa hii kumshukuru MwenyeziMungu, kwa ukarimu wake wa kutupa uhai, afya njema na nguvu, tukaweza kukutana tena katika Chombo hiki muhimu katika nchi yetu kwa lengo la kuwawakilisha wananchi wa Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika**, Pili napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa fursa ya kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu kwa ajili ya kuwasilisha hutuba ya Maoni ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kuhusiana na utekelezaji maagizo na ushauri wetu unaotokanayo na ripoti yetu ya Kamati kwa Wizara ya Maji, Nishati na Madini kwa mwaka 2021/2022.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa maelekezo ya Kanuni ya 109(18) ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2020 naomba kulijuilisha Baraza lako tukufu kwamba, Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati ya Baraza la Wawakilishi imepitia Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati yetu ya Mwaka 2021/2022 kwa Wizara ya Maji, Nishati na Madini ambapo katika Kipindi hicho Kamati yangu ilitoa Maagizo Ishirini (20) kwa Wizara hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** tukianza na Hoja zilizoelelekezwa kwa Mamlaka ya Maji pamoja na Idara ya Maji, Kamati inashauri kukamilishwa na kufuatwa kwa Mkakati wa Matumizi ya maji Zanzibar ili kudhibiti rasilimali hiyo, na kuhakikisha kila mmoja ananufaika na nishati hiyo. Aidha, Kamati inahimiza kuendelea kukamilisha mifumo ya Upatikanaji wa taarifa za ufuatiliaji wa mivujo ya maji, ujazo wa matangi pamoja na uzalishaji wa maji. Tunaomba mifumo hiyo ikamilishwe kwa Mikoa yote ya Zanzibar ili kubaini hitilafu yoyote ya mifumo ya maji katika maeneo yetu kwa njia za kisasa.

**Mheshimiwa Spika**, Kuhusu Miundombinu ya Maji, Kamati inaishauri Wizara kuzidi kusimamia ubora na vipimo sahihi vya mabomba yanayohitajika ili kujiepusha na tabia ya sasa ya kubadilisha ukubwa wa mabomba, muda mfupi baada ya kutumika kwa kuwa, huwa hayakidhi mahitaji yanayohitajika.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa ZECO na Idara ya Nishati, Kamati imefurahishwa na habari njema ya upembuzi yakinifu wa Miradi mitatu mikubwa ya kimkakati ya kuboresha nishati ya Umeme katika Visiwa vya Unguja na Pemba ikiwemo Ulazaji wa waya baharini wenye uwezo wa Megawati 200. Hatua hii itasaidia kwa kiasi kikubwa kuokoa hali iliyopo hivi sasa kwa waya wetu wenye uwezo wa Megawati 100 zikiwa hivi sasa '**zinayoyoma"** na kufikia matumizi ya megawati 77 na kuelekea kuzimaliza kabisa.

**Mheshimiwa Spika,** Tukifanya rejea ya ripoti za kamati zote zilizowahi kusimamia Wizara hii, tunabaini kwamba moja katika hoja inayojitokeza kila mwaka ni tatizo sugu la madeni hasa kwa taasisi za Serikali huku tukiwabana na kuwawekea mikakati mikubwa wananchi wa kawaida kusawazisha madeni yao ya umeme na maji.

**Mheshimiwa Spika,** Hadi tunapitia maagizo hayo ZECO inazidai taasisi mbali mbali jumla ya Shilingi za Kitanzania **Bilioni 52.4.** Kamati yetu kwa mara nyengine tena inazidi kutoa ushauri kwa serikali kuangalia uwezekano wa kusawazisha madeni hayo moja kwa moja kutoka Wizara ya Fedha kupitia "OC" zao.

**Mheshimiwa Spika**, Aidha Kamati yangu inahimiza kuharakishwa kwa suala la ZECO na TANESCO linalohusiana na Bei ya Shilingi 130 kwa unit moja ya Umeme kwani suala hilo limekuwa la muda mrefu.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati yangu, imefarajika kutokana na hatua ya Wizara kuweza kupambanuwa kazi za Wizara na kazi za ZURA, suala ambalo lilikuwa likileta mgongano wa majukumu kwa taasisi hizo. Kadhalika, Kamati inafurahi kusikia taasisi za ZECO na ZAWA nazo hivi sasa wanaendelea kushirikiana ipasavyo na ZURA katika hatua mbali mbali za kiutendaji, ikiwemo kuwasilisha mrejesho wa kaguzi zinazofanywa na ZURA. Kamati inasisitiza kila taasisi iheshimu majukumu ya mwenzake ili kutimiza malengo yaliyokusudiwa.

**Mheshiiwa Spika**, Kwa kumalizia Hotuba yangu napenda kugusia kidogo suala la Bohari ya Wesha na Mtoni. Kamati yangu inazidi kuwa na wasiwasi kwa kuendelea kutumika kwa matangi ya kuhifadhia mafuta katika maeneo hayo. Utafiti wa Kamati umebaini kwamba, matangi hayo hivi sasa tayari yameshamaliza muda wake wa matumizi (**life Spain**), hivyo mipango ya kuhamishiwa Ras Mkumbuu na Mangapwani iharakishwe kabla ya kutokea maafa katika maeneo hayo yanayoendelea kutumika hivi sasa.

**Mheshimiwa Spika,** Mwisho kabisa naomba kuchukua fursa hii kwa kuwashukuru Wajumbe wenzangu wa Kamati kwa mashirikiano yao waliyotoa kuanzia mwanzo hadi mwisho wa kazi ya kupitia utekelezaji wa maagizo haya, na kwa ruhsa yako naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo:

1. Mhe. Yahya Rashia Abdulla (MAMBA) - Mwenyekiti
2. Mhe. Hudhaima Mbarak Tahir - M/kiti
3. Mhe. Bahati Khamis Kombo - Mjumbe
4. Mhe. Mussa Foum Mussa - Mjumbe
5. Mhe. Kombo Mwinyi Shehe - Mjumbe
6. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu - Mjumbe
7. Ndg. Rahma Kombo Mgeni - Katibu
8. Ndg. Himid Haji Choko - Katibu

**Mheshimiwa Spika,** Nimalizie kwa kuwashukuru Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi kwa kunisikiliza kwa umakini na kwa utulivu mkubwa na naomba kuwasilisha.

(Mhe: Mussa Foum Mussa)
Kny: Mwenyekiti,
Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati,
Baraza la Wawakilishi,
Zanzibar.